**MAHALI SHULE ILIPO.**

Shule ya sekondari SUMVE (**Sumve High School**) ipo katika wilaya ya Kwimba, Mkoa wa Mwanza kilometa zipatazo 45 kusini – mashariki mwa jiji la Mwanza.

Usafiri wa kutoka jijini mwanza kuja sumve unapatikana stendi kuu ya Nyamuhongoro muda wa saa tano hadi saa nane mchana, na stendi ya kona ya kayenze (Kisesa) kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni. Ukifika kituo cha daladala Sumve ni mwendo kama wa dakika tano kwa mguu kufika shuleni.

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

1.1 **Sare ya shule**

i. Sketi 2 za marinda manane (mawili kila upande kulia na kushoto) kitambaa cha suti rangi ya dark blue, ziwe ndefu mpaka kwenye fundo za miguu.

ii. Shati 2 nyeupe zenye mikono mirefu (Tomato), hijabu 2 rangi nyeupe zilizoruhusiwa kisheria. (kwa waislam)

iii. Aje na shimizi au sidiria (rangi nyeupe au nyeusi tu).

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya Ngozi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi visivyokuwa na mapambo ya aina yoyote. Pia viatu vya **Juma na Rosa**)

v. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu (Stocking)

vi. Sweta 1rangi ya blue lenye nembo ya shule (pia anaweza kulipata shuleni kwa gharama ya shilingi 15,000)

vii. Tai 1 yenye nembo ya shule (anaweza kupata shuleni kwa gharama ya shilingi 6000)

viii. Track suit 1 rangi ya blue bahari yenye nembo ya shule (pia anaweza kuipata shuleni kwa gharama ya shilingi 25,000)

ix. Sare za michezo; Raba rangi nyeupe, soksi za bluu (stocking), jezi ya bluu kama zinavyoonekana kwenye kiambatanisho cha picha.

x. Sketi mbili za marinda mengi yaliyolalia upande mmoja za kushindia kitambaa cheusi cha suti, ziwe ndefu mpaka kwenye fundo za miguu.

xi. Suruali nyeusi ya kitambaa (sio jeans) kwa ajili ya kusomea wakati wa ‘prep’ usiku na sio vinginevyo.

xii. T-shirt 2 rangi ya kijivu zenye kola kwa ajiri ya kushindia zenye nembo ya shule (pia anaweza kuzipata shuleni kwa gharama ya shilingi 15,000 kwa kila 1

**1. 2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

i. Madaftari kumi **(counter books Quire 4)**

ii. Ream yenye karatasi aina ya Double A (1) kila muhula.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusu husika (kama inavyonekana kwenye kiambatisho)

iv. Scientific calculator kwa tahasusu ya EGM na HGE

v. Godoro kwa wanafunzi wa bweni la futi mbili na nusu. Aidha godoro linaweza kukodishwa shuleni kwa gharama ya shilingi 10,000 kwa mwaka kwa wachache watakao wahi kuripoti.

vi. Mashuka 2 (rangi ya pinki), blanket 1, chandarau 1 (nyeupe au pinki)

vii. Nguo za ndani za kutosha

viii. Vyombo vya chakula (Kontena lenye Mfuniko, kijiko na kikombe)

x. Ndoo 1 kubwa ya lita 20 kwa ajili ya kuhifadhia maji na ndogo 1 lita 10 kwa ajili ya kuogea na kufulia ( unaweza kuzipata maeneo ya shule).

xi. Sanduku la chuma (Tranka)kwa ajili ya kutunzia vitu

vyake xii. File tupu kwa ajili ya kutunzia taalifa zake shuleni

xiii. **Vifaa vya usafi kwa mchanganuo ufuatao**

**EGM -Jembe,chelewa,na soft bloom**

**HGE-Sabuni ya maji lt.5, chelewa na hard bloom**

**HGL-Koleo,chelewa na squeezer**

**HKL-Fyekeo,chelewa 2 na hard bloom**

**HGLi- Fyekeo,chelewa 2, na soft bloom**

**HGFa-Jembe na.sabuni ya maji lt.5**

**HGK- Koleo na.sabuni ya maji lt.5**

